# KATIBA YA HALMASHAURI YA WALEI KATOLIKI TANZANIA

## BARAZA LA MAASKOFU KATOLIKI TANZANIA

S.L.P. 9361
DAR ES SALAAM
TANZANIA

# YALIYOMO

VIFUPISHO........................................................................ UK. 2

HATI YA KUTANGAZA RASMI KATIBA YA
HALMASHAURI YA WALEI.................................................... UK. 3

UTANGULIZI ........................................................................ UK. 4

TAFSIRI NA UFAFANUZI ..................................................... UK. 5

SURA 1 - JINA, MALENGO NA MASHARTI .......................... UK. 10

SURA 2 - MUUNDO WA HALMASHAURI ............................. UK. 11

SURA 3 - VYAMA VYA KITUME NA JUMUIYA ZA KITUME .. UK. 13

SURA 4 - UONGOZI NA UCHAGUZI .................................... UK. 14

SURA 5 - WAJIBU WA VIONGOZI.......................................... UK. 18

SURA 6 - MIKUTANO NA VIKAO.......................................... UK. 23

SURA 7 - KAMATI MBALIMBALI ........................................ UK. 27

SURA 8 - MAISHA YA KIROHO............................................. UK. 31

SURA 9 - MALI YA HALMASHAURI .................................... UK. 36

SURA 10- KUBADILI KATIBA / KAULI YA MWISHO......... UK. 40

# VIFUPISHO

**AA:** **Apostolican Actuositatem -** Hati ya Mtaguso Mkuu wa Pili wa Vatikani juu ya Utume wa Walei.

CIC: **Condex luris Canonici** - Sheria za Kanisa.

**CL:** **Christifides Laici** - Barua ya Kitume ya Baba Mtakatifu Yohane Paulo II juu ya Wito na Utume wa Walei.

**EA:** **Ecclesia in Africa** - Barua ya kitume ya Baba Mtakatifu Yohane Paulo II kuhusu Sinodi ya Afrika.

**JNNK:** Jumuiya Ndogondogo za Kikristo.

**VJM:** Vyama, Mashirika na Jumuiya za Kitume.

## HATI YA KUTANGAZA RASMI KATIBA YA HALMASHAURI YA WALEI

Kila Mwanakanisa, kutokana na Ubatizo anao wajibu na haki ya kutenda Utume wake kadiri ya hali ya maisha. Na ili utume huu katika jamii ufanikiwe, Kanisa Katoliki linahitaji miongozo, taratibu na sheria za kuratibu utume wa makundi mbalimbali ya wanakanisa. Kundi mojawapo kubwa ni la Walei.

Katika karne mpya na milenia ni vyema kuwa na Katiba ya Halmashauri ya Walei Katoliki Tanzania iliyo mpya na inayoeleweka bila utata wowote. Lengo la katiba hii ni kuratibu shughuli zote za Halmashauri ya Walei, chombo cha Kitume kinachowaunganisha waamini. Walei katika wito na Utume wao wa kutakatifuza malimwengu. Chombo hiki ni tofauti na Halmashauri ya Walei, chombo cha kutakatifuza malimwengu. Chombo hiki ni tofauti na Halmashauri ya uchungaji (Pastoral Council rej. CD 20 na cc 511 - 514 CIC, ingawa vinafanyika pamoja.

Mwaka 1997 Maaskofu Katoliki Tanzania wakiongozwa na Ukarimu wa moyo wa upendo wa Kiuchungaji (CD 16) walipendekeza kwamba katiba ya awali ya Halmashauri ya Walei, ile ya mwaka 1975, ifanyiwe marekebisho ili iweze kukidhi mahitaji ya wakati huu.

Katiba hii mpya imejengwa juu ya msingi imara wa Maandiko Matakatifu, Mafundisho ya Mtaguso Mkuu wa Pili wa Vatikano na hasa hati juu ya utume wa Walei, Appostolicam Actuositatem, Sheria za Kanisa za Mwaka 1983, Barua ya Kitume ya Baba Mtakatifu Yohane Paulo wa II juu ya wito na utume wa Walei, Christifidels Laici na Barua ya Kitume inayohusu sinodi ya Afrika Ecclesia in Africa.

Kanisa la Tanzania kama ilivyo kanisa la kiulimwengu, limeingia karne mpya kwa nia ya Uinjilishaji wa kina huku likijua wazi kabisa kwamba Walei ni washiriki muhimu katika kazi hii (EA90).

Katika mabadiliko ya haraka yanayoikumba jamii ya sasa, tunafikiri kwamba katiba hii mpya inahitajika zaidi sasa huenda kuliko wakati mwingine wowote kuwa msaada mkubwa wa kuratibu shughuli zote za utume wa Walei wa kutakatifuza malimwengu (AA5,6).

Kwa sababu katiba hii imepitiwa na kuthibitishwa na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, tunatangaza rasmi ibara zote 93 za Katiba hii, na tunatamka kwamba, ibara hizo zitaongoza Halmashauri ya Walei, Vyama, Mashirika na Jumuiya zote za kitume za walei zenye hadhi ya kitaifa tangu tarehe 9 Januari 2004. Kwa kutangazwa rasmi ibara hizi 93, katiba nyingine zote za VMJ itabidi zirekebishwe ziendane na Katiba hii.

Imetolewa Kurasini, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, Novemba 7, 2003.

**+Mha. Askofu Severine NiweMugizi**
**RAIS**
**BARAZA LA MAASKOFU KATOLIKI TANZANIA**

## UTANGULIZI

Mtaguso Mkuu wa Pili wa Vatikano, katika hati yake inayohusu Utume wa Walei, unasema "Utume wa Walei hauwezi kutoweka kamwe katika kanisa" (AA1), kwa kuzingatia hilo na kwa kuzingatia kukua kwa teknolojia ya Utume wa Walei kwamba "Walei siyo tu wamo ndani ya kanisa bali vile vile wao ni Kanisa" (CL9). Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania tangu mwanzo wake limeenzi ushirikiano mzuri kati ya Walei na Hiararkia.

Aidha Kanisa Katoliki Tanzania linatambua kuwa Uinjilishaji wa Kanisa hauwezi kukamilika bila mchango wa Walei na kwamba Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo ni moja ya njia bora kabisa za Uinjilishaji (AMECEA 2002:41) na kujenga kanisa lililo Familia ya Mungu (EA 89).

Kwa misingi hiyo, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania limeruhusu kutumika kwa Katiba hii, itakayoratibu shughuli zote za HALMASHAURI YA WALEI chombo cha kitume kinachowaunganisha waamini Walei wote katika wito na Utume wao wa kushuhudia imani kwa kutakatifuza malimwengu (AA6&7).

Katiba hii vile vile ni kielelezo cha uongozi bora na shirikishi unaolenga katika kukuza na kulea karama za kila mmoja kama sehemu ya mwili wa Kristo na vile vile kuujenga mwili wa Kristo kwa pamoja kama familia ya Mungu (rej.1 Kor 12:12-31).

Hata hivyo, ili Walei waweze kutoa ushuhuda wa imani yao kwa ujasiri katika utume wao wa kutakatifuza malimwengu, ni lazima wajue imani yao vizuri. Ndiyo maana Maaskofu Katoliki Tanzania wanaporuhusu kutumika kwa katiba hii, kwanza wanawaalika Walei, waisome na waijue vizuri katiba hii. Vilevile, wanawahimiza walei wote wapende kujifunza na kujua mambo yanayohusu imani yao na hivyo wawe mashahidi wa kweli wa imani yao katika Tanzania na hata mwisho wa nchi (rej. Mdo 1:8).

Uongozi katika Halmashauri ya Walei katika ngazi yoyote ile siyo mamlaka, basi Utume, hivyo unadai sala na moyo wa kujitoa kwa mfano wa Kristo mwenyewe ambaye hakuja kutumikiwa bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi (Mk 10:45).

Hivyo basi tunawahimiza Viongozi Walei wadumu katika sala na mazoezi mbalimbali ya kiroho ili waweze kuimarika katika Utume wao (Mt.26:41) kwa sababu wao vilevile ni Kanisa, watakapotenda yale yote yanayohusu Utume wao, wasisubiri sifa, wala malipo bali waseme "sisi tu watumwa wasio na faida tumefanya tu yaliyotupasa kufanya" (Lk 17:10)

**+Askofu Jacob V. Koda**
ASKOFU MWENYEKITI
IDARA YA UTUME WA WALEI
BARAZA LA MAASKOFU KATOLIKI TANZANIA

# TAFSIRI NA UFAFANUZI

**1. WALEI**

Ni waamini wote ukiondoa, makleri na wale wenye maisha ya Wakfu. Hawa ni waamini ambao. Kwa ubatizo wao na kipaimara wameunganishwa na Kristo na kufanya Taifa la Mungu, wanashiriki katika kazi ya Kristo ya ukuhani, unabii na ufalme, binafsi na kwa pamoja na wametumwa kuwa mawakili waaminifu kuyafanya malimwengu na taasisi ziongozwe na roho ya Injili.

**II. HALMASHAURI YA WALEI**

Ni chombo cha kitume kinachowaunganishwa walei wote katika Jumuiya ndogondogo za kikristo, (vijiji/mitaa) vigango/ parokia/jimbo na taifa. Ni chombo cha kitume kilichoundwa kwa ajili ya kushauri juu ya ustawi wa Utume wa Walei, na kinachoendeshwa na walei wenyewe waliochaguliwa kihalali chini ya ushauri na uongozi wa jumla wa viongozi hiararkia (AA2d)

**III. KWA UJUMLA KATIBA HII INATAMBUA HALMASHAURI WALEI**

Katika jumuiya ndogondogo za kikristo, (vijiji/mitaa) vigango/ parokia/jimbo na taifa. Kila moja ya ngazi hizo ina mazingira yake na kwa sababu hiyo kila sehemu inaweza kuwa na Halmashauri ndogo ndogo ili mradi Walei wote wanaunganishwa na chombo hiki kutekeleza lengo lililowekwa.

**IV. HALMASHAURI KUU YA WALEI:**

Ni chombo cha juu kabisa cha utendaji wa Halmashauri Walei katika Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo, vijiji / mitaa,vigango, parokia, jimbo na taifa. Hiki ndicho chombo cha kupendekeza

sera na mipango. Utendaji wa chombo hiki utafanyika kwa kushirikisha utendaji wa vyombo vingine vya kanisa kadiri ya utaratibu wa sheria za Kanisa Katoliki. Sera na mipango ya chombo hiki, vitapata nguvu za kiutendaji baada ya ridhaa ya mamlaka za juu za Kanisa yaani, Paroko, Askofu au Baraza la Maaskofu.

V. **KAMATI TENDAJI**

Ni chombo cha HALMASHAURI YA WALEI chenye jukumu la kutekeleza yale yaliyoamuliwa katika vikao vya HALMASHAURI KUU na kupata ridhaa ya uongozi wa Kanisa. Ni chombo pia kinachobuni mipango ya utendaji, sera za Halmashauri na kuwakilisha kwenye vikao vya juu yake kwa majadiliano na uamuzi. Kama ilivyoelezwa katika No.4 uamuzi huu hupelekwa kwenye vyombo vya juu vya mamlaka ya Kanisa kama mapendekezo. Katika vikao vyake vyombo hivyo hutoa uamuzi wa kurudishwa kwa Halmashauri Walei kwa ajili ya utekelezaji.

VI. **KAMATI NDOGO NDOGO**

Ni kamati zinazoundwa katika ngazi yoyote ile ya uongozi wa HALMASHAURI YA WALEI na kwa kushirikiana na vyombo vingine vya kanisa kushughulikia masuala fulani maalum ya kiutume.

Vyombo hivyo ni kama vile idara mbalimbali katika ngazi ya Parokia, Jimbo au Taifa, vyama / mashirika / jumuiya za kitume au vitengo vya utendaji vya wenye maisha ya wakfu.

VII. **VYAMA VYA KITUME:**

Hivi ni vyama vilivyoanzishwa na baadhi ya wakristo makleri, walei na wenye maisha ya wakfu na kuidhinishwa na uongozi wa kanisa kwa lengo la kutekeleza utume wa aina fulani. Baadhi ya vyama hivi vyaweza kuwa vimeanzishwa katika kanisa la mahali katika ngazi ya Parokia, Jimbo na baadaye kutambuliwa kitaifa na hivyo kuwa vya kitaifa n kijimbo. Vingine vimeanzishwa katika maeneo fulani lakini vikapata bahati ya kuenea katika kanisa la ulimwengu.

Sifa kuu mbili za vyama / mashirika / jumuiya za kitume ni kuwa vimetambuliwa na kukubaliwa na uongozi wa kanisa la mahali au ulimwengu, na pili vinatekeleza utume wake kulingana na karama ya mwanzilishi wake (AA.19).

VIII. **PAROKIA**

Makao makuu ya Parokia yatakuwa pia makao makuu ya Halmashauri ya Walei katika ngazi ya Parokia. Mshauri wa jumla katika ustawi wa utume wa walei atakuwa Paroko au msaidizi wake. Ieleweke kuwa viongozi wa Halmashauri hawaitwi viongozi wa Parokia katika ngazi hii, bali ni viongozi wa Halmashauri Walei Parokia kama ilivyo katika ngazi ya Jimbo na Taifa. Kwa hiyo, Mwenyekiti ataitwa Mwenyekiti wa Halmashauri Walei Parokia, vilevile viongozi wengine wote.

IX. **JIMBO**

Makao makuu ya Jimbo yatakuwa pia makao makuu ya HALMASHAURI YA WALEI kijimbo na viongozi wataratibu shughuli zote za HALMASHAURI YA WALEI katika ngazi hiyo.

X. **TAIFA**

Ofisi ya taifa ya Halmashauri Walei itakuwa pale ambapo zipo ofisi za Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, isipokuwa kama imekuwa vingine na Baraza la Maaskofu. Shughuli za Halmashauri Walei Taifa zitafanyika katika Ofisi ya Idara ya Utume wa Walei ya Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania.

XI. **MALIMWENGU**

Ni mambo yote ya maisha, hali ya familia, uchumi, utamaduni, ufundi wa kila aina, mambo ya siasa uhusiano kati ya mataifa na mengine.

XII. **MAZINGIRA**

Ni mambo yote yanayoonekana ambayo binadamu anayatumia kwa faida au hasara yake.

XIII. **TAASISI**

Ni kama vile shule, vyuo, idara, n.k.

XIV. **VIONGOZI HIERARKIA**

Mashemasi, Mapadre na Maaskofu.

XV. **VIONGOZI WALEI**

Viongozi wa Halmashauri ya Walei au viongozi wa vyama vya kitume.

XVI. **JUMUIYA NDOGONDOGO ZA KIKRISTO**

Ni namna ya kuwa Kanisa leo kwa wakristo katika ngazi ya msingi ya familia na kwa msingi wa ujirani kimakazi, waliokubaliana kushirikiana ukristo wao na wito wao wa kueneza Injili kimatendo. Mkusanyiko wa wakristo wenye nia moja kwa njia ya familia zao za kikristo ndio unaunda jumuiya ndogondogo za Kikristo ambazo ndizo kanisa la msingi.

IXVII. **USHAURI**

Ni neno / maneno, tendo / matendo yanayohusu kuelekeza, kuonya, kushawishi, kuweka mipaka yanayotolewa na mtu / watu / kikundi kwa mtu mwingine watu wengine / kikundi kwa lengo la kufanya utendaji uwe bora na unaokubaliwa kwa kadiri ya taratibu za kisheria na kiimani zilizowekwa kikanisa katika ngazi fulani.

# SURA YA KWANZA

## JINA, MALENGO NA MASHARTI

1. **JINA**

Halmashauri ya Walei Katoliki Tanzania, kwa kifupi 'Halmashauri Walei'. Makao makuu yatakuwa Bakanja TEC Laity Centre, Sitakishari - Ukonga S.L.P. 9361 - Dar es Salaam.

2. **MALENGO**

2.1 Kujenga nguzo imara ya kanisa ili kwamba viongozi walei na walei wote kwa ujumla kwa kushirikiana na uongozi Hierarkia wanatenda kwa ajili ya kueneza mpango mtakatifu wa wokovu kwa watu wote, katika nyakati zote na mahali pote.

2.2 Kutekeleza Utume wa Walei ambao unalenga katika kuyafanya malimwengu, na taasisi tunamoishi viongozwe na roho ya Injili.

2.3 Kutoa ushuhuda wa matendo yatokanayo na imani ya kikristo katika malimwengu.

2.4 Kuwezesha Walei, kutokana na karama za Sakramenti walizopokea, kushiriki kikamilifu katika Uinjilishaji wa kina mfungamano na mipango yote ya Kanisa, katika harakati za kuujenga Mwili wa Kristo.

3. **MASHARTI**

Mkatoliki Mlei yeyote aliye na umri wa kuanzia miaka 18 mwenye akili timamu ni mshiriki na anastahili kuonesha nia yake na kushiriki kuhudhuria mikutano, kupiga kura na kupigiwa kura, na kuwajibika kadiri ya karama yake binafsi, pamoja na wengine katika Kanisa na Jamii.

# SURA YA PILI

## MUUNDO WA HALMASHAURI WALEI

Muundo wa HALMASHAURI ya WALEI utaanzia ngazi ya Jumuiya ndogo ndogo za Kikristo hadi Taifa kama ifuatavyo:-

4.1 **HALMASHAURI** inayoundwa na Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo ni wawakilishi waliochaguliwa na jumuiya ya baba familia na mamafamilia wote, pamoja na watoto familia wenye umari kuanzia miaka 18.

4.2 **HALMASHAURI YA WALEI MTAA / KIJIJI**
Inaundwa na wenyeviti na kamati tendaji za HALMASHAURI JNNK, wenyeviti wa vyama vya kitume.

4.3 **HALMASHAURI YA WALEI KIGANGO**
Inaundwa na kamati tendaji za Halmashauri Mtaa / Kijiji katika eneo husika na wenyeviti wa vyama vya kitume.

4.4 **HALMASHAURI YA WALEI PAROKIA**
Inajumuisha wenyeviti wa wajumbe wengine wawili kutoka miongoni mwa Kamati Tendaji ya Halmashauri mtaa/kijiji/kigango kulingana na mazingira ya Parokia husika na wenyeviti wa vyama vya kitume. Paroko ni mjumbe rasmi katika ngazi hii.

4.5 **HALMASHAURI YA WALEI JIMBO**
Inajumuisha wenyeviti na wajumbe wengine angalau wawili (hasa Katibu na Mhazini) kutoka miongoni mwa Kamati Tendaji kutoka kila Halmashauri Parokia na wenyeviti wa vyama vya kitume. Askofu, Mkurugenzi wa Utume wa Walei, Katibu Mtendaji wa Idara ya Utume wa Walei ni wajumbe rasmi, idara

au tume za Katekesi, Liturujia, Miito, Uchungaji, Afya, Haki na Amani na Elimu zaweza kualikwa pia.

## 4.6 HALMASHAURI YA WALEI TAIFA

Inaundwa na wenyeviti wa Halmashauri majimbo na Wenyeviti wa vyama vya kitume ngazi ya Taifa, Askofu Mwenyekiti wa Idara ya Utume wa Walei na Katibu Mtendaji wa Idara Utume wa Walei. Idara au Tume za Katekesi, Uchungaji, Liturijia, Elimu, Haki na Amani zaweza kualikwa pia.

# SURA YA TATU

## VYAMA VYA KITUME NA JUMUIYA ZA KITUME

5. Vyama / Mashirika na Jumuiya za kitume (VMJ) zitafanya kazi zake chini ya mwavuli wa HALMASHAURI YA WALEI katika ngazi yoyote ile. Mwavuli kwa upande mmoja unaundwa na kukamilishwa kwa njia ya uwepo na utendaji wa vyama vya Kitume.

6. Kwa upande mwingine bila kuingia utendaji wa VMJ za kitume, HALMASHAURI YA WALEI itashirikiana navyo na itavishauri, kuvitia moyo na kuviimarisha pale inapobidi.

7. VJM za kitume zitajitegemea kiutendaji na kikarama, ila zinaweza kutumia hati ya usajili ya HALMASHAURI YA WALEI katika utendaji wake wa nje na ndani ya Kanisa inapobidi.

8. Wawakilishi wa VMJ za Kitume watahudhuria mikutano ya HALMASHAURI YA WALEI katika ngazi zote kama wajumbe wengine na wanaweza kuchagua ama kuchaguliwa kushika uongozi katika nafasi yoyote ile.

# SURA YA NNE

## UONGOZI NA UCHAGUZI

## SEHEMU A: SIFA ZA KIONGOZI

9. Kwa ujumla, sifa za KIONGOZI sharti zikubaliane na kuimarishwa na mshauri ya Injili. Kwa hiyo, kiongozi atakayechaguliwa awe Mkatoliki, mwenye umri usiopungua miaka 18, awe na akili timamu, awe mtendaji hodari wa kazi, awe mwenye tabia njema kwa maneno na matendo yake, awe amechaguliwa na Walei wenzake, awe amekubalika na uongozi hiararkia, asiwe na kizuizi chochote cha Sakramenti na akubalike na JNNK anayotoka isipokuwa kama yupo katika nafasi ya uongozi unaopita katika ngazi husika. Ni vema atakayechaguliwa kuwa kiongozi awe pia na uzoefu katika utendaji wa shughuli za Chama, Shirika au Jumuiya ya Kitume.

9.1 Kiongozi katika ngazi ya Taifa na Jimbo lazima awe na sifa za ziada kama vile uzoefu wa ofisi atakayoshika na kiwango cha elimu kinachomruhusu kuwasiliana na ngazi za juu za Kanisa na hata kuweza kuwakilisha Taifa/Jimbo katika vikao vya juu zaidi.
Kwa upande wa Mwenyekiti Jimbo au Taifa sifa nyingine zinaweza kuongezwa na Baraza la Maaskofu kulingana na mahitaji ya wakati na mazingira.

9.2 Afisa Mtendaji kama mwajiriwa, ni lazima awe pia na elimu ya kutosheleza kutekeleza kazi zake vizuri kwa ufanisi. Lugha ya Taifa Kiswahili na Kiingereza ni lazima kwake kwa ajili ya hulka ya kazi za Uafisa Mtendaji.

9.3 Mhasibu / Mweka Hazina ni lazima awe na ujuzi na uzoefu wa masuala ya fedha kadiri ya fani ya uhasibu.

## SEHEMU B: UCHAGUZI WA VIONGOZI

10. Viongozi wanachaguliwa katika ngazi zote ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Katibu Msaidizi na Mhazini (Mhazini Msaidizi)

11. Afisa Mtendaji wa Halmashauri ya Walei ni mwajiriwa na katika mkutano wa uchaguzi athibitishwe na mkutano unaohusika. Dhana ya uwakili itaongoza uwajibikaji wa Afisa Mtendaji wa Halmashauri Walei ngazi husika.

12. Uchaguzi wa viongozi utafanyika kwa kura ya siri na kila mjumbe ana haki ya kura moja.

13. Viongozi wanastahili kuchaguliwa ni wale waliomo ndani ya mkutano wa uchaguzi, isipokuwa kama mjumbe asiyekuwepo ameacha maelezo ya kuridhisha na iwapo wenzake, Paroko, Mkurugenzi au Askofu wanamwona anafaa.

14. Kwa ajili ya ufanisi wa kiutendaji, mjumbe anayechaguliwa kuchukua uongozi wa nafasi fulani kiutendaji katika ngazi ya parokia, jimbo au Taifa, ajiuzulu uongozi wa ngazi ya chini yake kwa nafasi ile ile badala yake achaguliwe mjumbe mwingine katika kipindi kisichozidi miezi mitatu. Jambo hili litafanyika kwa idhini ya uongozi.

14.1 Mjumbe anayejiuzulu uongozi wa ngazi ya chini anabaki mjumbe halali katika vikao vyote vya ngazi hiyo aliyojiuzulu.

## SEHEMU C: MUDA WA UONGOZI

15. Viongozi wa HALMASHAURI YA WALEI katika ngazi zote watashika nafasi kwa muda wa miaka mitatu (3) waweza kuchaguliwa tena lakini isizidi mara tatu mfululizo katika nafasi au ngazi ile ile.

## SEHEMU D: KUACHA NA KUACHISHWA UONGOZI

16. Kiongozi yeyote asiyehudhuria mikutano mitatu mfululizo bila sababu ya msingi atapoteza kiti chake na wa chini yake atakaimu kiti hicho hadi uchaguzi mdogo ufanyike katika kipindi cha miezi mitatu kujaza nafasi hiyo. Iwapo aliyepoteza kiti ni Mhazini, kiongozi mwingine atateuliwa na HALMASHAURI ya ngazi husika kushika nafasi hiyo hadi uchaguzi mdogo utakapofanyika katika muda wa miezi mitatu kujaza nafasi yake.

16.1 Kiongozi asiyeitisha mikutano miwili mfululizo ya kikatiba kama inavyoelezwa katika sura ya sita, bila sababu ya msingi atapoteza kiti chake na wa chini yake atakaimu kiti hicho hadi uchaguzi mdogo ufanyike katika kipindi kisichozidi miezi mitatu kujaza nafasi hiyo.

17. Kiongozi anaweza kuacha nafasi ya uongozi kwa kujiuzulu ili mradi atoe taarifa ya kimaandishi kwa Mwenyekiti / Mshauri / Mlezi mwezi mmoja kabla ya kuacha uongozi. Kiongozi ambaye haendelei kutoa huduma kwa sababu yoyote ile isipokuwa kifo, atapaswa kukabidhi mali yote aliyotumia kutendea kazi kama ni ya HALMASHAURI YA WALEI, mahali alipotoa taarifa ya kujiuzulu au kwa mdhamini wa mamlaka iliyomwachisha huduma ya uongozi na kutoa taarifa yake ya utendaji kimaandishi.

18. Kiongozi anaweza kuacha uongozi kwa kuwajibishwa na Halmashauri ya Walei au uongozi Hierarkia ngazi husika ikiwa itabainika kuwa sifa za uongozi kadri ya mashauri ya Injili zimepurukushwa.

18.1 Kuwajibishwa kwa kiongozi katika ngazi ya JNNK, Kigango na Parokia, kutafanyika kwa kuhusisha uongozi Hierarkia wa ngazi ya juu yake.

18.2 Iwapo kiongozi atakufa au atapata uhamisho au kupata matatizo ya kiafya nafasi yake itakaimiwa kwa muda usiozidi miezi mitatu na uchaguzi mdogo ufanyike kujaza nafasi yake.

# SURA YA TANO

## WAJIBU WA VIONGOZI

## SEHEMU A: WAJIBU WA JUMLA

19. Wajibu wa viongozi wa Halmashauri katika ngazi zote ni:-
    - 19.1 Kudumisha Utume wa Walei na kuimarisha maisha ya kiutakatifu miongoni mwa Walei na kuwahiza Walei kushiriki katika kuujenga Mwili wa Kristo.
    - 19.2 Kustawisha utume wa familia na uinjilishaji wa kina.
    - 19.3 Kushauri na kushiriki katika ujenzi wa Kanisa mahalia, Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo wakiunganika katika utendaji na uongozi Hiararkia.
    - 19.4 Kujenga na kudumisha moyo wa sala na ibada sahihi miongoni mwa Walei.
    - 19.5 Kustawisha vikundi mbalimbali vya kitume katika maeneo yao.
    - 19.6 Kushirikiana na uongozi Hiararkia katika ngazi yoyote ya Halmashauri ya Walei katika kutekeleza majukumu ya Kanisa.
    - 19.7 Kuhamasisha shughuli za kimaendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kadiri ya mtazamo wa kanisa.
    - 19.8 Kuwawezesha na kushauri juu ya uongozi bora katika jamii.
    - 19.9 Kushirikiana na taasisi na mashirika mengine katika masuala yote ya maendeleo ya binadamu, mwili na roho kwa kuzingatia kanuni za Kanisa.
    - 19.10 Kushirikiana kikamilifu na kwa kutumia miundo iliyowekwa na Kanisa katika kulinda na kutetea uhai, heshima na haki za binadamu.

## SEHEMU B: WAJIBU WA VIONGOZI WA KAMATI TENDAJI

20. **MWENYEKITI: (MAKAMU WAKE)**

20.1 Kuwa mhimili wa utendaji wa HALMASHAURI YA WALEI.

20.2 Kuwa msemaji wa HALMASHAURI WALEI.

20.3 Kuongoza mijadala katika mikutano.

20.4 Kupitisha na kuidhinisha dondoo za mkutano.

20.5 Kutoa uamuzi wa mwisho katika masuala fulani mawazo yanapogongana kadiri ya busara yake na kwa kumhusisha mshauri wa kiroho wa Halmashauri ya Walei husika.

20.6 Kufuatilia utekelezaji wa mazimio ya mkutano HALMASHAURI YA WALEI.

20.8 Kutoa taarifa za mara kwa mara za utekelezaji wa shughuli kwa HALMASHAURI YA WALEI na uongozi Hairarkia ngazi husika.

20.9 Kushirikisha viongozi wa vyama vyote vya kitume katika mikutano ya HALMASHAURI na utendaji.

21. **KATIBU (KATIBU MSAIDIZI)**

21.1 Kuwa Mtendaji Mkuu wa HALMASHAURI WALEI

21.2 Kuijua na kuelezea katiba na kuitumia kwa busara bila kupoteza lengo.

21.3 Kumshauri Mwenyekiti katika masuala yote ya kiutendaji.

21.4 Kutayarisha dondoo za mkutano.

21.5 Kuitisha vikao kwa mujibu wa Katiba hii.

21.6 Iwapo kuna semina / kongamano, kuandaa mambo yote yatakiwayo kwa ushirikiano na viongozi wenzake.

21.7 Kuandaa mahali pa mikutano na mambo muhimu yatakiwayo.

21.8 Kuwakaribisha wageni kutoka taasisi mbalimbali.

21.9 Kuandaa muhtasari wa mkutano na kusoma kinachofuata.

21.10 Kupokea na kuhifadhi kumbukumbu zote.

21.11 Kushughulikia barua zote za kiofisi.

21.12 Kufuatilia utekelezaji wa maazimio yote ya mkutano.

21.13 Kuandaa taarifa mbalimbali na kuziwasilisha sehemu husika.

21.14 Kupokea taarifa mbalimbali kutoa vyama vya kitume na kuziunganisha na kuziwasilisha sehemu husika.

22. **MHAZINI**

22.1 Kutunza mali za HALMASHAURI pamoja na kumbukumbu zake zote.

22.2 Kuweka vizuri hesabu za mapato na matumizi.

22.3 Kudhibiti matumizi.

22.4 Kubuni mipango na mbinu za kuzalisha mali kwa ushirikiano na viongozi wenzake.

22.5 Kufuatilia utekelezaji wa maazimio yahusuyo fedha na miradi.

22.6 Kutoa taarifa ya mapato na matumizi katika vikao husika.

22.7 Kuandaa bajeti.

23. **AFISA MTENDAJI**

Halmashauri Walei katika ngazi yeyote ile, kadiri itakavyoona inafaa, kwa kutegemea uwezo wake wa kifedha, inaweza kuwa na Afisa Mtendaji sharti uthibitishwe na Askofu Jimbo.

Atashika nafasi hiyo kwa muda wa miaka mitatu.

**Majukumu yake ni:**

23.1 Kufanya kazi kama ofisa mkuu wa halmashauri.

23.2 Kuratibu shughuli za kila siku za halmashauri.

23.3 Kufanya kazi zote za kiofisi.

23.4 Kuwa kiungo cha utendaji kwa wajumbe wa kamati tendaji za vyama / mashirika / jumuiya za Kitume.

23.5 Kushirikiana kwa karibu na Katibu Mtendaji / Mkurugenzi wa Idara ya Utume wa Walei ya Kikanisa ngazi husika.

23.6 Kubuni na kupendekeza majukumu ya idara ya utume wa walei pamoja na mambo mengine atakayoelekezwa.

## 24. KAMA MJUMBE HALMASHAURI NA MJUMBE KAMATI

**Majukumu yake ni:-**

24.1 Kuwasilisha mawazo ya watu mkutanoni na kuwapelekea watu maamuzi ya mkutano.

24.2 Kushiriki kikamilifu katika mijadala licha ya kutokuwa na kura ya maamuzi.

24.3 Kupokea na kutekeleza kazi anazopewa na vikao

24.4 Kuwajibika katika majukumu ya pekee anayoteuliwa kufanya.

# SURA YA SITA

## MIKUTANO NA VIKAO

## SEHEMU A: MKUTANO MKUU WA JNNK

25. Kutakuwa na mkutano mkuu JNNK utakaofanyika mara tatu kwa mwaka.
26. Wajumbe wa mkutano huo ni wanajumuiya wote wa JNNK katika Jumuiya hiyo ambazo ni pamoja na wanachama na viongozi wote wa vyama vya kitume katika ngazi hiyo.
27. Majukumu ya mkutano huo ni:-
    - 27.1 Kupokea taarifa na maendelezo kutoka ngazi za juu za uongozi na kuyatekeleza.
    - 27.2 Kutoa maoni na mapendekezo kwa ngazi za juu kupitia vyombo husika.
    - 27.3 Kupokea na kupitisha taarifa ya fedha na makisio ya mwaka ya jumuiya yao.
    - 27.4 Kuchagua viongozi wa kamati tendaji wakati wa mkutano wa uchaguzi.

**SEHEMU B: MKUTANO WA HALMASHAURI YA WALEI JNNK**

28. Itakutana mara sita kwa mwaka yaani mara moja kila miezi miwili.

29. Wajumbe ni:-
    - 29.1 Kamati tendaji JNNK
    - 29.2 Mwenyekiti wa Chama cha Kitume katika JNNK
    - 29.3 Mwakilishi wa kila familia katika JNNK husika
    - 29.4 Makatibu wa kamati ndogo ndogo

30. Majukumu yake yatakuwa kupokea taarifa na kubuni / kupanga mikakati ya utekelezaji.

**SEHEMU C: HALMASHAURI MTAA/ KIJIJI/ KIGANGO PAROKIA NA JIMBO**

31. Halmashauri Mtaa/Kijiji, Kigango na Parokia watafanya mikutano yao mara mbili kwa mwaka. Halmashauri jimbo itafanya mkutano wake mara moja kwa mwaka.

32. Mikutano na vikao katika ngazi ya Parokia, Jimbo na Taifa, vitakuwa na jukumu la kutoa maoni kwa kumsaidia Askofu Jimbo kupitisha uamuzi katika masuala yanayoligusu Kanisa. Askofu wa Jimbo na Baraza la Maaskofu litakuwa na sauti ya mwisho juu ya masuala yanayolihusu Kanisa mahalia. Ushauri wa vikao vya Halmashauri Walei kwa ngazi zote utakuwa na nguvu ya kushauri na wala sio nguvu ya uamuzi.

**Wajumbe ni:**

32.1 Kamati Tendaji
32.2 Wenyeviti wa VJM za Kitume katika ngazi husika
32.3 Makatibu wa kamati ndogo ndogo
32.4 Wenyeviti na wajumbe wawili kama ifuatavyo:
32.4.1 Kijiji/Mtaa: Kutoka kila Halmashauri JNNK.
32.4.2 Kigango: Kutoka kila Halmashauri mtaa au kijiji katika ngazi hii Katekista ni mjumbe rasmi.

32.4.3 Parokia: Wenyeviti kutoka kamati tendaji kila Halmashauri Walei Kijiji Mtaa/ Kigango kulingana na Mazingira.

32.4.4 Jimbo: Wajumbe watatu kutoka kila kamati tendaji Halmashauri Walei Parokia (Mwenyekiti wa Halmashauri Parokia - lazima awepo).

33. **JIMBO**

33.1 Katika ngazi ya jimbo, pamoja na wajumbe waliotajwa hapo juu, wafuatao ni wajumbe rasmi:

33.2 Askofu Jimbo na Mkurugenzi wa Utume wa Walei.

33.3 Wakurugenzi wa idara za Katekesi, Liturujia, Kiuchungaji, Haki na Amani na Elimu.

33.4 Wajumbe wasio rasmi / wasio na kura ya uamuzi

33.4.1 Mwakilishi wa Masista

33.4.2 Mwakilishi wa Mabradha

33.4.3 Waalikwa

34. **SEHEMU D: HALMASHAURI KUU (TAIFA)**

Halmashauri Kuu itakutana angalau mara moja kwa mwaka

34.1 Wajumbe Rasmi

34.1.1 Kamati tendaji

34.1.2 Makatibu wa kamati ndogo ndogo

34.1.3 Wenyeviti wa Halmashauri ya majimbo

34.1.4 Wenyeviti wa vyama vya Kitume (T)

34.1.5 Askofu Mwenyekiti wa idara ya utume wa Walei

34.1.6 Katibu Mtendaji wa idara ya Utume wa Walei

34.2 Wajumbe wasio rasmi

34.2.1 Makatibu watendaji wa idara ya Katekesi, Liturujia, Kiuchungaji, Elimu, Caratas, Afya na Katibu wa "Tanzania Catholic Association of Sisters" wanaweza kualikwa.

34.2.2 Wajumbe waalikwa kutoka ndani na nje ya nchi.

**SEHEMU E: TAARIFA ZA MIKUTANO**

35. Mikutano ya kamati tendaji itolewe taarifa siku saba kabla ya siku ya mkutano.
36. Mikutano ya Halmashauri JNNK, Kigango cha Parokia, taarifa itolewe siku kumi na nne kabla ya siku ya mkutano.
37. Taarifa ya mkutano wa Halmashauri jimbo itolewe siku thelathini kabla ya mkutano.
38. Taarifa ya mkutano wa Halmashauri Kuu Taifa itolewe angalau siku sitini kabla ya siku ya mkutano.

**SEHEMU F: IDADI HALALI YA MAHUDHURIO**

39. Idadi inayofika nusu ya wajumbe wa mkutano wowote wa Halmashauri inatosha kuhalalisha mkutano.

**SEHEMU G: MIKUTANO MAALUMU**

40. Mikutano ya aina hii inaweza kufanyika wakati wowote katika ngazi inayohusika mradi itolewe taarifa siku zisizopungua ishirini na moja kabla ya siku ya mkutano kutegemea na mazingira.
41. Mikutano ya aina inaweza kuitishwa na mwenyekiti kwa kushirikiana na kamati tendaji, mshahuri au mlezi.

    Au wajumbe wengine watano wa Halmashauri au Askofu Mwenyekiti wa Idara ya Utume wa Walei au Katibu Mtendaji wa Idara kwa idhini ya Askofu Mwenyekiti.

# SURA YA SABA

## KAMATI MBALIMBALI

## SEHEMU A: KAMATI TENDAJI

42. Kamati Tendaji katika ngazi zote zitakuwa walau mara moja kila mwezi na zitakuwa na wajumbe wafuatao:-
    - 42.1 Mwenyekiti
    - 42.2 Makamu Mwenyekiti
    - 42.3 Katibu
    - 42.4 Katibu Msaidizi
    - 42.5 Mhazini Msaidizi (Mhazini)
    - 42.6 Mshauri / Mlezi, Paroko, Mkurugenzi wa Idara (J) / Katibu Mtendaji wa idara (T)

43. **Majukumu ya Kamati Tendaji**
    - 43.1 Kushughulikia matukio ya siku kwa siku
    - 43.2 Kutekeleza maazimio, maagizo na maelekezo yote yaliyopitishwa katika vikao mbalimbali.
    - 43.3 Kubuni na kuwasilisha mapendekezo ya utendaji kwa halmashauri Walei.
    - 43.4 Kuunganisha kazi mbalimbali za vyama vya kitume katika ngazi husika.
    - 43.5 Kuteua wajumbe wasiozidi wanne kuunda kamati ndogo ndogo
    - 43.6 Kuratibu kazi za kamati ndogo ndogo
    - 43.7 Kujenga mahusiano na taasisi na mashirika mengine.

43.8 Kuandaa makisio ya Bajeti ya mwaka kwa majadiliano na idhini ya Halmashauri Kuu.

**SEHEMU B: KAMATI NDOGO NDOGO**

Zitakutana walau mara moja kila mwezi kabla ya Kamati Tendaji mshahuri / mlezi, Paroko, Mkurugenzi wa Idara (J) au Katibu Mtendaji wa Idara (T) ni wajumbe rasmi.

**B.1 KAMATI YA MIPANGO, UCHUMI NA FEDHA**

44. Wajumbe
    - 44.1 Mwenyekiti ni mhazini wa Kamati Tendaji.
    - 44.2 Wajumbe wengine wanne kutoka miongoni mwa Halmashauri katika ngazi husika.
    - 44.3 Paroko / Mkurugenzi (J) Katibu Mtendaji wa Idara (T)
    - 44.4 Mweka Hazinaa (J).

**45. Majukumu:**
   - 45.1 Kushirikiana na kuzingatia ushauri wa Katibu Mtendaji / Mkurugenzi wa Idara kuhusu masuala ya mali ya Halmashauri / Kanisa.
   - 45.2 Kuangalia na kusimamia mali ya Halmashauri / Kanisa.
   - 45.3 Kubuni mikakati ya kupata fedha za kuendeshea shughuli za Halmashauri / Kanisa.
   - 45.4 Kupendekeza bajeti ya Halmashauri na kudhibiti matumizi.

**B.2 KAMATI YA MALEZI NA FAMILIA**

46. Wajumbe:
    - 46.1 Mwenyekiti wa kamati tendaji atakuwa Mwenyekiti wa Kamati hii.
    - 46.2 Wajumbe wanne kutoka miongoni mwa Halmashauri.
    - 46.3 Katibu Mtendaji / Mkurugenzi wa Liturujia na Idara katika ngazi husika anaweza kualikwa.

**Majukumu yake ni:-**

46.3.1 Kuratibu na kusimamia malezi ya watoto na vijana kwa njia mbalimbali.

46.3.2 Kuhamasisha uanzishwaji wa shule za chekechea na awali.

46.3.3 Kuratibu mafundisho na malezi endelevu ya vijana na watu wa ndoa.

46.3.4 Kuratibu na kusimamia mafunzo ya uzazi wa mpango kulingana na mafundisho ya Kanisa.

46.3.5 Kushauri, kwa kusaidiana na Paroko, katika masuala ya ndoa na familia.

## B.3 KAMATI YA IBADA NA LITURUJIA

47. Wajumbe:

47.1 Makamu mwenyekiti wa kamati Tendaji atakuwa Mwenyekiti wa kamati hii.

47.2 Wajumbe wengine wanne kutoka miongoni mwa Halmashauri Walei.

47.3 Katibu Mtendaji / Mkurugenzi wa idara katika ngazi husika anaweza kualikwa.

47.4 **Majukumu yake:**

47.4.1 Kuratibu ufundishaji wa sala na ibada mbalimbali za Kanisa

47.4.2 Kupanga na kusimamia shughuli za huduma mbalimbali Kanisani.

47.4.3 Kuongoza sala na tafakari ya neno la Mungu

## B.4 KAMATI YA ELIMU YA DINI, MAFUNDISHO YA KANISA NA TEOLOJIA

48. Wajumbe:

48.1 Katibu Msaidizi ndiye Mwenyekiti wa kamati hii.

48.2 Wajumbe wanne kutoka miongoni mwa Halmashauri Walei

48.3 Mkurugenzi / Katibu Mtendaji, Idara ya Elimu katika ngazi husika anaweza kualikwa.

48.4 Mkatekista.

48.5 **Majukumu yake ni:**

48.5.1 Kuwezesha ufundishaji Biblia Takatifu na maandiko mengine kuhusu Kanisa

48.5.2 Kuweza ufundishaji wa sakramenti mbalimbali za Kanisa

48.5.3 Kuwezesha na kusimamia uekumene na mahusiano na dini nyingine.

48.5.4 Kuratibu mafundisho ya dini shuleni.

## B.5 KAMATI YA HAKI NA AMANI

48.6 **Wajumbe:**

48.6.1 Katibu wa Kamati Tendaji atakuwa Mwenyekiti wa kamati hii.

48.6.2 Wajumbe wengine wanne kutoka miongoni mwa HALMASHAURI Walei

48.6.3 Katibu kamisheni ya Haki na Amani katika ngazi husika anaweza kualikwa.

48.7 **Majukumu yake:**

48.7.1 Kuratibu ufundishaji wa mafundisho Jamii ya Kanisa.

48.7.2 Kubuni programu za kuwezesha roho ya Injili kupenyeza katika malimwengu na taasisi.

48.7.3 Kuratibu na kufundisha haki na wajibu mbalimbali za watu.

48.7.4 Bila kuathiri utendaji wa kamati husika, mjumbe yeyote katika kamati ndogo ndogo haruhusiwi kuhudumia zaidi ya kamati moja isipokuwa anaweza kuhudhuria kama mwalikwa.

# SURA YA NANE

## MAISHA YA KIROHO

49. Ni wajibu wa kila mwanahalmashauri kutambua kuwa ametumwa na Kristo kumshuhudia kwa njia ya maneno na matendo. Kama vile Kristo alivyokuwa Mtakatifu katika maisha yake, kila Mwanahalmashauri aweke mbele maisha ya sala, asali daima bila kuchoka na awelekeze wenzake kusali.
50. Mikutano yote ya Halmashauri itaanza kwa sala inayoongozwa kwa neno la Mungu, kufanyika katika roho ya sala na kumalizika kwa sala.
51. Halmashauri katika ngazi zote itatenga angalau siku mbili katika mwaka kwa ajili ya mafungo na tafakari ya utume katika maisha halisi. Halmashauri Walei katika ngazi zote itajiwekea utaratibu wa kufanya tafakari ya kiroho mara kwa mara kadiri ya inavyowezekana.
52. Kila mwanahalmashauri awe na Biblia Takatifu na awe na ari ya kuitumia na kutafakari vifungu anavyovisoma.
53. Katika sikukuu ya Pentekoste, kamati tendaji katika ngazi ya Parokia kwa kushirikiana na paroko watayarishe na kutoa mahubiri kulingana na dhamira kuu ya mwaka unaohusika inavyotolewa kwa kushirikisha idara ya utume wa walei.

54. Kadiri ya mazingira, JNNK ziteue siku moja katika mwaka kwa ajili ya kukusanyika na kumega mkate pamoja wote washiriki upendo wa kristo miongoni mwao.

55. Uongozi Hierarkia unaundwa na Makleri yaani Maaskofu, Mapadre na Mashemasi.

55.1 Mlei atakayetumwa na uongozi Hiarakia kutimiza wajibu fulani kwa nafasi yake kama kiongozi katika Utume wa Walei, wanakanisa watawajibika kumpokea na kuzingatia anayotenda kwa utume aliokabidhiwa. Mlei huyu ana ushirikiano na uongozi Hiarakia katika kuuwezesha uongozi hiarakia kuliongoza Kanisa la Kristo akibaki katika hali yake ya Kilei.

55.2 Mapadri, Mashemasi na Watawa katika kutimiza Utume wao kati ya Walei, watabaki na mamlaka yao ya Kisakramenti/kiwito na ya kiofisi.

56. Kwa ujumla viongozi hiarakia watahusiana na Halmashauri Walei kama wachungaji na kondoo (Yn.10:14). Hawa ni washauri wa jumla katika masuala yote ya Halmashauri Walei na Utume wa Wale katika ngazi zote za uongozi wa Kanisa. Viongozi hiarakia wanaalikwa kustawisha utume wa Walei (AA22).

**SEHEMU A: JNNK / KIGANGO / MTAA / PAROKIA**

57. Paroko ndiye mshauri na mkolezaji wa jumla wa utume wa Walei katika ngazi hii.

58. Katika Mkutano wa uchaguzi wa viongozi wa Halmashauri Walei, Paroko atashauri juu ya sifa za wagombea na kusimamia uchaguzi huo yeye mwenyewe binafsi au mwakilishi wake.
59. Kwa kupitia Halmashauri Walei, Paroko ataratibu na kusimamia utendaji wa vyama vya kitume katika eneo lake la uchungaji

**SEHEMU B: JIMBO**

60. Kiongozi Mkuu katika ngazi hii ni Askofu. Utume wa Walei na Utume wa makleri na watawa unapata ridhaa ya utendaji kwa njia ya Askofu Jimbo.
61. Askofu Jimbo ndiye mshauri wa jumla katika masuala yote ya utume wa walei.
62. Mkurugenzi wa utume wa walei jimboni huteuliwa na Askofu kwa ajili ya kuratibu kazi za utume wa walei jimboni.
63. Majukumu yake:
    - 63.1 Kumshauri Askofu katika masuala yote yahusuyo Utume wa Walei.
    - 63.2 Kuwa mkuu wa idara ya utume wa walei na atatekeleza majukumu kwa kushirikiana kwa karibu zaidi na Kamati Tendaji ya Halmashauri Walei ili kuboresha utendaji wa idara.

64. Idara ya utume wa walei jimboni huundwa na Mkurugenzi wa Utume wa Walei washauri wa vyama / mashirika, jumuiya za kitume na kamati tendaji za Halmashauri Walei na vyama, mashirika, jumuiya za kitume katika ngazi hiyo.

65. Katika mkutano wa uchaguzi, Mkurugenzi wa Utume wa walei. Jimboni ndiye msimamizi na mwenye kutoa kauli ya mwisho kwa niaba ya Askofu endapo kauli hiyo haihitaji kupitishwa na Askofu.

**SEHEMU C: TAIFA**

66. Idara ya utume wa Walei ya Baraza la Maaskofu ndicho chombo cha kitaifa katika kushauri na kusimamia utendaji wa Utume wa Walei.

67. **Majukumu ya Idara ya Utume wa Walei ni:**
    - 67.1 Kushauri Baraza la Maaskofu katika masuala ya Utume wa Walei.
    - 67.2 Kushauri na kutia moyo kazi za Halmashauri ya Walei na VMJ.
    - 67.3 Kuratibu na kusimamia utendaji wa kazi za kitume katika ngazi hiyo.

68. Watendaji wa Idara ni Askofu Mwenyekiti wa Idara na Katibu Mtendaji wa Idara, waratibu wa vitengo vya idara, washauri wa vyama / mashirika ya kitume na kamati tendaji za halmashauri vyama / mashirika ya kitume.

69. Askofu Mwenyekiti wa Idara ndiye msemaji wa masuala yote yahusuyo utume wa Walei katika vikao vya Baraza la Maaskofu. Pia atawakilisha masuala yote ya utume wa Walei katika ngazi za kimataifa pale ambapo Walei wenyewe hawahusiki katika vikao hivyo.

70. Katibu Mtendaji wa idara ni wakili wa Askofu Mwenyekiti. Atatekeleza majukumu yake kwa karibu.

Zaidi na Kamati Tendaji ya Halmashauri Walei ili kuboresha utendaji wa pamoja kiidara.

71. Katibu Mtendaji wa Idara ya utume wa walei atakuwa kiungo kati ya idara ya utume wa walei na idara nyingine za Baraza la Maaskofu kwa upande mmoja na kati ya Sekretariati ya Baraza la Maaskofu na Halmashauri Walei na VMJ za kitume kwa upande mwingine. Yeye ni msemaji wa masuala yote ya Utume wa Walei katika vikao / mikutano ya wakuu wa idara.

72. Katika mikutano ya uchaguzi wa Halmashauri Walei / Vyama / Mashirika ya kitume Askofu Mwenyekiti wa Idara au Katibu Mtendaji wa idara ndiye mwenye kutoa neno la mwisho.

**SEHEMU D: WASHAURI WA KIROHO (CHAPLAINS)**

73. Hawa huteuliwa na Askofu au Baraza la Maaskofu katika ngazi ya Jimbo au Taifa kwa ajili ya kusimamia maisha ya kiroho ya wanachama wa utume (mahususi).

**74. Majukumu ni:**

74.1 Kupendekeza dhamira za kiroho kwa kila mwaka kwa kushirikiana na chama/shirika husika.

74.2 Kuongoza mafungo, tafakari na ibada mbalimbali

74.3 Kusimamia utekelezaji wa utume kwa mujibu wa roho ya mwanzilishi wa utume kwa mujibu wa roho ya mwanzilishi wa utume husika.

74.4 Kushauri juu ya maisha asili na ya uchaji kwa wanachama/ wanashirika.

74.5 Bila kuathiri utendaji wao, mipango ya utendaji ya washauri wa kiroho iratibiwe.

Pamoja na mipango mingine ya kitume kiidara ili kujenga umoja wa kiidara

74.6 Washauri wa kiroho wawashirikishe wakuu wa idara (wakurugenzi (J) na katiba mtendaji wa idara (T) kama mashauri wa jumla wa mipango yote kabla haijatekelezwa.

# <u>SURA YA TISA</u>

## SEHEMU A: MALI YA HALMASHAURI

75. Halmashauri inaweza kuwa na mali inayohamishika ama isiyohamishika. Mali hii itamilikiwa kadiri ya sheria za kanisa (CIC 1983, Kitabu V) na sheria za nchi.

75.1 Askofu Jimbo anaweza kutunga sheria ndogo iliyo chini ya sheria za kanisa juu ya mali ya Halmashauri ya Walei.

75.2 Askofu, kwa nafasi yake katika Kanisa mahalia, atahakikisha kuwa mali ya Halmashauri Walei iko na inatumika kwa ajili ya kazi na malengo ya Kanisa Katoliki.

75.3 Mali hii ni lazima ilenge kufanikisha Utume wa Walei na Ustawi wao.

75.4 Mali itakayozidi kiwango cha kawaida itatunzwa kwa kufuata sheria na maelezo ya Baraza la Maaskofu na Kanisa kwa ujumla.

75.5 Halmashauri Walei haitajiingiza katika umiliki na uendeshaji wa miradi ya kiuchumi inayopingana na mtazamo wa utume wa kanisa katoliki mahalia ama kiulimwengu.

75.6 Kabla ya kumiliki mali yenye kuzidi kiwango kinachowekwa na Maaskofu, Halmashauri Walei lazima itafute ushauri na ruhusa kutoka kwa Askofu Jimbo.

**SEHEMU B: UPOKEAJI NA UWEKAJI WA FEDHA**

76. Stakabadhi zitolewe kuhusu michango, zawadi na mapato yote ya Halmashauri.
77. Fedha hizo hata mali nyingine zinazohamishika na sizizohamishika zitatunzwa chini ya uangalizi wa kituo cha Kanisa, kama vile Parokia, jimbo au Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania
78. Halmashauri inaweza kuwa na akaunti yake ya benki ikiwa jambo hilo ni lazima sana na linaongeza ufanisi. Watakaotia saini za kutoa fedha kutoka Benki ni wale watakaokubaliwa na uongozi hiarakia.
79. Mapato na matumizi yote ya Halmashauri yatatayarishwa na kutekelezwa chini ya mwavuli wa Parokia, Jimbo na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) ili Kanisa linufaike.

**SEHEMU C: KUKOPA NA KUKOPESHA**

80. Halmashauri inaweza kukopa na kukopesha, pia kufanya biashara kupata mapato ya kuendesha shughuli zake baada ya kushauriwa na kupata idhini ya viongozi Hiararkia. Ulipaji wa mikopo utafanywa na Halmashauri bila kutegemea mali ya Parokia, Jimbo ama TEC.

**SEHEMU D: KUSHITAKI NA KUSHITAKIWA**

81. HALMASHAURI inaweza kushiriki au kushitakiwa kwa mambo yale yasiyo ya Parokia, Jimbo, TEC au Kanisa katoliki kwa ujumla. Masuala ya Imani na maadili ya kanisa katoliki hayataweza kufikishwa mahakamani na Halmashauri Walei. Halmashauri Walei haina uwezo kuliwakilisha katika mahakama kwa kesi inazolihusu Kanisa kwa ngazi yoyote ile kama haitakuwa imeagizwa kuwa mwakilishi wa Kanisa.

**SEHEMU E: MWAKA WA HALMASHAURI**

82. Mwaka wa HALMASHAURI Utakuwa tangu tarehe Mosi Julai mpaka tarehe thelathini ya mwezi Juni, mwaka unaofuata kulingana na mwaka wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania.

**SEHEMU F: UHUSIANO**

83. Lazima kuwepo ushirikiano na uhusiano mwema kati ya HALMASHAURI na vyombo vingine vya kanisa ya wokovu wa wanadamu. Halmashauri Walei itajenga uhusiano kwa kuzingatia taratibu za utendaji na mahusiano zinazowekwa na Idara ya Utume wa Walei Taifa au jimbo pamoja na sheria za Kanisa kwa ujumla.

84. HALMASHAURI YA WALEI kwa kufuata matamko ya wachungaji wa kanisa itaweka uhusiano mzuri na ushirikiano kati yake na HALMASHAURI WALEI za nchi nyingine. Itajenga undugu kamili kati yake na makundi ya kikristo na madhehebu yasiyo ya Kikatoliki, yasiyo ya Kikristo na hata yale yasiyo ya kidini.

## SEHEMU G: WADHAMINI

85. Wadhamini wa fedha na mali za Halmashauri ni Paroko, Askofu na Baraza la Maaskofu

## SEHEMU H: KANUNI

86. HALMASHAURI YA WALEI kwa ngazi zote itaongozwa na katiba hii itakayoanza kutumika tarehe itakayoamuliwa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania.

**86.1** Katiba hii ni moja kwa HALMASHAURI YA WALEI TANZANIA, katika vikao vyake mbalimbali kama vile. JNNK/ MTAA/ VIGANGO / PAROKIA NA JIMBO / TAIFA HALMASHAURI ya mahali inaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kila siku mradi kanuni hizo zisivuke mipaka ya katiba hii.

# SURA YA KUMI

## KUBADILI KATIBA / KAULI YA MWISHO

87. Taarifa ya miezi mitatu, kwa maandishi, lazima itumwe kwa HALMASHAURI KUU kuhusu mabadiliko yoyote au nyongeza za Katiba hii kabla ya Mkutano Mkuu wa HALMASHAURI na Taifa kutoka wajumbe wasiopungua kumi na HALMASHAURI Taifa.
88. Kamati Tendaji, italeta mapendekezo ya mabadiliko au nyongeza hizo mbele ya Halmashauri Kuu ya Taifa ili zijadiliwe.
89. Theluthi mbili ya wajumbe waliohudhuria mkutano huo wa Taifa walikubali mabadiliko yoyote au nyongeza hizo zitajumuishwa rasmi katika Katiba hii.
90. Mabadiliko au / nyongeza zitaweza kuwa halali zikipendekezwa wakati wa mkutano Mkuu wa HALMASHAURI YA WALEI na kujadiliwa na kukubaliwa na theluthi mbili ya wajumbe wa Taifa waliohudhuria Mkutano huo.
91. Marekebisho yaliyofanywa yatakuwa na nguvu za kiutendaji baada ya kukubaliwa na kupitishwa na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania.
92. KAULI YA MWISHO: Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania litatoa kauli ya mwisho kuhusu katiba hii.
93. Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania linaweza kusimamisha na kutaka mabadiliko ya Katiba hii wakati wowote ule inapokuwa lazima.